# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MUHTASARI WA SOMO LA URAIA NA MAADILI

## ELIMU YA MSINGI

## DARASA LA III-VII

© Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, 2015

Toleo la Kwanza, 2015
Toleo la Pili, 2016
Toleo la Tatu, 2019

ISBN9 78-9987-09-061-7

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam

Simu: +255 22 2773005/+255 22 277 1358
Nukushi: +255 22 2774420
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Taasisi ya Elimu Tanzania. (2015). Muhtasari wa Somo la Uraia na Maadili Elimu ya Msingi Darasa la III-VII. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kutafsiri andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

## Yaliyomo


Dibaji ........ iv
Orodha ya majedwali ........ v
1.0 Utangulizi........ 1
2.0 Maelezo ya jumla kuhusu Mtaala........ 2
2.1 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VII ........ 2
2.2 Umahiri wa Elimu ya Msingi Darasa la III-VII........ 3
2.3 Malengo ya kufundisha Somo la Uraia na Maadili........ 3
2.4 Umahiri mkuu na umahiri mahsusi katika Somo la Uraia na Maadili ........ 4
2.5 Ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Uraia na Maadili ........ 5
2.6 Upimaji wa ujifunzaji ........ 5
3.0 Maudhui ya muhtasari........ 5
3.1 Umahiri mkuu........ 5
3.2 Umahiri mahususi........ 5
3.3 Shughuli za mwanafunzi........ 6
3.4 Vigezo vya upimaji........ 6
3.5 Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi ........ 6
3.6 Idadi ya vipindi........ 6
3.7 Maudhui ya Darasa la III........ 8
3.8 Maudhui ya Darasa la IV........ 22
3.9 Maudhui ya Darasa la V........ 40
3.10 Maudhui ya Darasa la VI........ 61
3.11 Maudhui ya Darasa la VII........ 85

## Dibaji

Elimu bora ni haki ya kila Mtanzania. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuwa ikiboresha Mtaala wa Elimu ya Msingi kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa ni bora na inayomwandaa mwanafunzi kumudu maisha katika mazingira yake. Muktadha huu umewezesha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuboresha mchakato wa kufundisha na kujifunza Somo la Uraia na Maadili kwa kuandaa muhtasari huu.

Maudhui katika muhtasari huu yameandaliwa katika mtindo wa kukuza umahiri katika Somo la Uraia na Maadili. Serikali inategemea Muhtasari huu ujenge umahiri wa kutambua misingi ya uzalendo katika jamii yetu, kubaini mabadiliko yanayotokea katika mazingira, kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali na kutambua matukio yanayotokea katika jamii na mahali pengine ulimwenguni. Hata hivyo, umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) unaendelea kupewa msisitizo katika Somo la Uraia na Maadili.

Ninachukua nafasi hii kuwahimiza wadau wote wa elimu kutumia muhtasari huu katika kutekeleza na kufuatilia mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaendelea kupokea maoni ya kuboresha muhtasari huu kutoka kwa wadau wote. Maoni yote yapelekwe kwa Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Elimu Tanzania. Mwisho, napenda kuwashukuru washiriki wote kutoka taasisi, asasi, na makundi mbalimbali ambao wamewezesha kazi hii kukamilika kwa ufanisi.



.........................................................

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa<br>
**Kaimu Kamishna wa Elimu**<br>
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi katika Somo la Uraia na Maadili ........ 4
Jedwali Na. 2 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi darasa la III........ 7
Jedwali Na. 3 Maudhui ya darasa la III ........ 8
Jedwali Na. 4 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi darasa la IV ........ 21
Jedwali Na. 5 Maudhui ya darasa la IV ........ 22
Jedwali Na. 6 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi darasa la V ........ 39
Jedwali Na. 7 Maudhui ya darasa la V ........ 40
Jedwali Na. 8 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi darasa la VI ........ 60
Jedwali Na. 9 Maudhui ya darasa la VI ........ 61
Jedwali Na.10 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi darasa la VII ........ 84
Jedwali Na.11 Maudhui ya darasa la VII ........ 85

## 1.0 Utangulizi

Muhtasari wa Somo la Uraia na Maadili umeandaliwa kwa kuzingatia Mtaala wa Elimu ya Msingi mwaka 2015, toleo la tatu mwaka 2019, wenye kuzingatia ujenzi wa umahiri kwa mwanafunzi.

Somo la Uraia lilikuwa linafundishwa katika shule za msingi tangu uhuru kama Somo la Siasa. Mwaka 1996, Somo la Siasa liliunganishwa kwenye Somo la Maarifa ya Jamii. Mwaka 2007, Somo la Uraia lilianza kufundishwa kama somo linalojitegemea. Elimu ya maadili ilianza kufundishwa katika Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA). Elimu hii ilitolewa katika somo lililoitwa Ujenzi wa Haiba. Baada ya mpango huo wa MEMKWA wahitimu waliweza kubadilika kitabia na kimwenendo. Kutokana na mafanikio yaliyopatikana kwenye mpango wa MEMKWA, Wizara ya Elimu na Ufundi iliamua kuanzisha Somo la Haiba na Michezo katika shule za msingi ili kukuza maadili. Lengo lilikuwa kumpa mtoto stadi za maisha na za ushindani zitakazomwezesha kujithamini, kuthamini utu, kujiamini, kuthubutu na kufanya uamuzi sahihi.

Sababu za kuanzisha Somo la Uraia na Maadili ni pamoja na:

a) Somo la Uraia na Maadili ni somo linalojitegemea. Maswali yanayoulizwa katika Somo la Maadili na majibu yanayotolewa ni tofauti na maswali na majibu yanayotolewa na masomo mengine. Katika maadili hatujiulizi tu kuhusu kanuni zinazobainisha uzuri na ubaya wa matendo ya binadamu bali pia tunajiuliza ni jinsi gani binadamu anastahili au anapaswa kuishi. Kwa maneno mengine, katika Somo la Uraia na Maadili tunajiuliza maisha mazuri ni yapi? Kuishi vizuri maana yake ni nini? Ubaya ni nini? Tunawezaje kuishi kama binadamu? Majibu ya maswali haya hutolewa na Somo la Uraia na Maadili na si somo jingine;

b) somo hili linalenga kumjengea mwanafunzi tabia inayokubalika ya kuheshimu na kuthamini jamii, uwajibikaji, ustahimilivu, uadilifu pamoja na kudumisha amani;

c) tafiti zilibainisha kuwa somo hili linatakiwa lijitegemee. Aidha tafiti hizo zilionesha kuwa umahiri anaojenga mwanafunzi katika Somo la Uraia unaendana vizuri na maadili. Hii imesababisha kuanzishwa kwa Somo la Uraia na Maadili. Utafiti huo pia ulihusisha uzoefu wa nchi mbalimbali duniani

Muhtasari huu wa Somo la Uraia na Maadili umeandaliwa kutokana na Mtaala wa Elimu ya Msingi wa mwaka 2016. Muhtasari huu umegawanywa katika sehemu kuu tatu (3): Sehemu hizo ni utangulizi, maelezo ya jumla ya mtaala pamoja na maudhui ya muhtasari.

## 2.0 Maelezo ya jumla ya mtaala wa elimu ya msingi

Mtaala wa elimu ya msingi umeundwa na sehemu mbalimbali ambazo zinaonesha kwamba mtaala ni dhana inayojumuisha mambo mengi ambayo yanahusiana. Sehemu hii inawasilisha baadhi ya vipengele vya mtaala ambavyo ni Malengo ya Elimu ya Msingi, Umahiri wa Elimu ya Msingi, Umuhimu wa Somo la Uraia na Maadili, Malengo ya Somo la Uraia na Maadili, Umahiri Mkuu na Mahususi, Ufundishaji na Ujifunzaji na Upimaji wa Ujifunzaji.

## 2.1 Malengo ya elimu ya msingi darasa la III-VII

Elimu ya Msingi ina madhumuni ya kuwapatia walengwa maarifa, stadi na mwelekeo unaohitajika kwa maendeleo ya Watanzania. Malengo makuu ya elimu ya msingi ni kumwezesha mwanafunzi:

a) kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana;
b) kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Kiswahili.
c) kufahamu misingi ya utawala wa sheria.
d) kuthamini utamaduni wa Kitanzania na wa jamii nyingine.
e) kukuza uwezo wa mwanafunzi kufikiri, kubuni, na kutatua matatizo.
f) kutambua umuhimu wa maadili, uadilifu na uwajibikaji kama misingi ya raia mwema.
g) kushiriki katika shughuli za michezo na sanaa pamoja na kuthamini kazi za kisanii.
h) kubaini na kukuza vipaji na vipawa vyake.
i) kuthamini na kupenda kufanya kazi.
j) kutambua, kuthamini na kutumia sayansi na teknolojia; na
k) kumwandaa mwanafunzi kwa ngazi nyingine ya elimu pamoja na kuandaa ari ya kujifunza kusiko na kikomo.

## 2.2 Umahiri wa elimu ya msingi darasa la III-VII

Umahiri wa Elimu ya Msingi umejikita katika kumwandaa mwanafunzi kuwa na uwezo wa:

a) kuwasiliana kwa ufasaha kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa kuzungumza na kuandika;
b) kusoma kwa kujiamini na kufahamu maandishi sahili;
c) kutumia dhana na kanuni za kihisabati katika maisha ya kila siku;
d) kutumia stadi za kisayansi, kiteknolojia na ufundi katika maisha halisi ya kila siku;
e) kuthamini utamaduni wake na wa jamii nyingine;
f) kujali tofauti za kiimani na kiitikadi katika jamii;
g) kushiriki katika michezo na shughuli za kisanii;
h) kujiheshimu na kuheshimu wengine;
i) kutenda matendo ya kizalendo;
j) kushiriki katika kazi mbalimbali zinazoendana na umri wake;
k) kushiriki katika shughuli zinazokuza uwezo wake wa kufikiri kimantiki na kiyakinifu; na
l) kushirikiana na wengine kwa kufanya matendo yanayostahili/yanayofaa katika jamii

## 2.3 Malengo ya kufundisha Somo la Uraia na Maadili

Malengo makuu ya ufundishaji Somo la Uraia na Maadili kwa mwanafunzi wa Darasa la III-VII ni:

a) kuelewa asasi na taasisi za kisiasa na za kijamii na kazi zake katika utawala wa kidemokrasia;
b) kutafsiri, kuthamini na kuheshimu vitambulisho vya taifa letu, katiba, muundo na uendeshaji wa Serikali;
c) kuelewa misingi ya kidemokrasia katika shughuli za utawala na uongozi;
d) kutambua wajibu wao, kuheshimu na kutetea haki za binadamu na usawa wa sheria;
e) kuelewa na kushiriki katika shughuli za utawala, uongozi, ulinzi na usalama wa taifa katika jamii wanamoishi;
f) kuwa wabunifu na kuweza kubaini na kuchambua matatizo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na kubuni mbinu za kuyatatua;
g) kutambua tofauti baina ya watu zitokanazo na itikadi na hali zao na kujenga uvumilivu kuhusu tofauti hizo;
h) kujenga moyo wa umoja wa kitaifa na ushirikiano baina ya jamii za Tanzania na jamii za mataifa mengine; na
i) kuishi kwa kutumia elimu ya masuala mtambuko

## 2.4 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahsusi katika Somo la Uraia na Maadili

**Jedwali Na. 1: Umahiri wa Somo la Uraia na Maadili**

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 1.Kuheshimu jamii | 1.1 Kujipenda na kuwapenda watu wengine.<br>1.2 Kuipenda na kujivunia shule yake.<br>1.3 Kuipenda Tanzania kwa kuenzi tunu za nchi na asili yake. |
| 2. Kuithamini jamii | 2.1 Kujijali na kuwajali wengine.<br>2.2 Kutunza mazingira.<br>2.3 Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii. |
| 3. Kuwa mwajibikaji | 3.1 Kulinda rasilimali na maslahi ya nchi.<br>3.2 Kusimamia majukumu yanayomhusu nyumbani na shuleni.<br>3.3 Kutii sheria na kanuni katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.<br>3.4 Kuwa na nidhamu.<br>3.5 Kushirikiana katika kutekeleza majukumu ya nyumbani na shuleni. |
| 4. Kuwa mstahimilivu | 4.1 Kuvumilia katika maisha ya kila siku.<br>4.2 Kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya.<br>4.3 Kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu. |
| 5. Kuwa mwadilifu | 5.1 Kuaminika katika jamii.<br>5.2 Kutimiza majukumu yake kwa uwazi na ukweli.<br>5.3 Kusimamia haki. |
| 6. Kudumisha amani | 6.1 Kuchangamana na watu wenye asili tofauti.<br>6.2 Kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti.<br>6.3 Kujenga urafiki mwema na mataifa mengine. |

## 2.5 Ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Uraia na Maadili

Kufundisha na kujifunza Somo la Uraia na Maadili kutasisitiza ujenzi wa umahiri kwa kutumia mbinu shirikishi. Mbinu hizi zitamfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji na mwalimu kuwa mwezeshaji. Kufundisha na kujifunza kutajikita katika kumjengea mwanafunzi uwezo wa kupata umahiri unaokusudiwa. Somo la Uraia na Maadili litamsaidia mwanafunzi kujenga na kukuza maadili yanayoakisi utamaduni wa Mtanzania na dunia kwa ujumla.

## 2.6 Upimaji wa ujifunzaji

Upimaji ni sehemu muhimu katika machakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kupima kutamwezewa mwalimu kubaini kufikiwa kwa ujenzi wa umahiri uliokusudiwa. Kupima kutafanyika kwa kutumia zana za aina mbalimbali. Zana hizi zitajumuisha mitihani ya kuandika, hojaji, uchunguzi makini, maswali ya ana kwa ana, mkoba wa kazi na orodha hakiki. Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi utahusisha upimaji endelevu.

## 3.0 Maudhui ya muhtasari

Maudhui ya muhtasari yamepangwa kwa kila darasa na yanajumuisha umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na mwanafunzi, vigezo vya upimaji, upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi na idadi ya vipindi kwa kila umahiri mahususi.

## 3.1 Umahiri mkuu

Huu ni uwezo wa kutenda jambo kwa usahihi na kwa ufanisi unaokusudiwa kwa muda fulani. Umahiri mkuu hujengwa na umahiri mahususi, ambao nao hujengwa na mwanafunzi kwa kutenda shughuli mbalimbali.

## 3.2 Umahiri mahususi

Huu ni uwezo ambao hujengwa na mwanafunzi kwa kutenda kwa ufanisi shughuli mbalimbali zilizolengwa ndani ya muktadha wa umahiri mkuu.

### 3.3 Shughuli za mwanafunzi

Hivi ni vitendo ambavyo mwanafunzi anapaswa kuvitenda ili kufikia umahiri mahususi uliokusudiwa kwa kuzingatia uwezo na darasa husika.

### 3.4 Vigezo vya upimaji

Hivi ni viwango vya ufanisi wa utendaji wa mwanafunzi ili kufikia umahiri mahususi uliokusudiwa.

### 3.5 Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi

Hivi ni viwango vya ufikiwaji wa vigezo vya upimaji kwa kila shughuli iliyokusudiwa kutendwa na mwanafunzi.

### 3.6 Idadi ya vipindi

Haya ni makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutenda mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi 5 kwa wiki. Hata hivyo, mapendekezo haya ya idadi ya vipindi yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

## 3.7 Darasa la III

**Jedwali Na. 2:** Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi darasa la III

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 1. Kuheshimu jamii | 1.1 Kujipenda na kuwapenda watu wengine.<br>1.2 Kuipenda na kujivunia shule yake.<br>1.3 Kuipenda Tanzania kwa kuenzi tunu za nchi na asili yake. |
| 2. Kuithamini jamii | 2.1 Kujijali na kuwajali wengine.<br>2.2 Kutunza mazingira na vilivyomo.<br>2.3 Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii. |
| 3. Kuwa mwajibikaji | 3.1 Kulinda rasilimali na maslahi ya nchi.<br>3.2 Kusimamia majukumu yanayomhusu nyumbani na shuleni.<br>3.3 Kutii sheria na kanuni mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.<br>3.4 Kuwa na nidhamu binafsi.<br>3.5 Kushirikiana katika kutekeleza majukumu ya nyumbani na shuleni. |
| 4. Kuwa mstahimilivu | 4.1 Kuandaa kanuni za kufikia malengo katika maisha ya kila siku.<br>4.2 Kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya.<br>4.3 Kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu. |
| 5. Kuwa mwadilifu | 5.1 Kuaminika katika jamii.<br>5.2 Kutimiza majukumu yake kwa uwazi na ukweli.<br>5.3 Kusimamia haki. |
| 6. Kudumisha amani | 6.1 Kuchangamana na watu wenye asili tofauti.<br>6.2 Kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti.<br>6.3 Kujenga urafiki mwema na mataifa mengine. |

**Jedwali Na. 3: Maudhui ya darasa la III**

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 1. Kuheshimu jamii | 1.1 Kujipenda na kuwapenda watu wengine | a) Kutenda matendo ya kuheshimu watu wote | Matendo ya kuheshimu watu wote yanatendwa kwa usahihi | Anatenda matendo ya kuheshimu kwa watu wachache anaowafahamu kwa karibu | Anatenda matendo ya kuheshimu watu anaowafahamu na wengine | Anatenda matendo ya kuheshimu watu wote | Anatenda matendo ya kuheshimu watu wote na kuwahamasisha wenzake kutenda matendo ayo. | 16 |
| | | b) Kutenda matendo ya kujipenda | Matendo ya kujipenda yanatendwa ipasavyo | Anatenda matendo ya kujipenda kwa kushurutishwa | Anatenda matendo ya kujipenda kwa kuiga wengine | Anatenda matendo ya kujipenda | Anatenda matendo ya kujipenda na kuwashawishi wengine kujipenda | |
| | | c) Kutenda matendo yenye kuonesha upendo kwa watu wote | Matendo yenye kuonesha upendo kwa watu wote yanatendwa ipasavyo | Anatenda matendo machache yenye kuonesha upendo kwa baadhi ya watu anaowafahamu tu | Anatenda matendo yenye kuonesha upendo kwa baadhi ya watu anaowafahamu | Anatenda matendo yenye kuonesha upendo kwa watu wote | Anatenda na anashauri wenzake kufanya matendo yenye kuonesha upendo kwa watu wote | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 1.2 Kuipenda na kujivunia shule yake | a) Kufahamu shule yake | Mambo yanayohusu shule yake yanafahamika kikamilifu | Anafahamu mambo machache sana kuhusu shule yake | Anafahamu mambo kadhaa kuhusu shule yake | Anafahamu shule yake kikamilifu | Anafahamu kikamilifu kuhusu shule yake na kuwafahamisha wengine | 12 |
| | | b) Kutunza mazingira ya shule yake | Utunzaji wa mazingira ya shule yake unafanyika kwa ari na kujituma | Anatunza mazingira ya shule yake kwa kushurutishwa | Anatunza mazingira ya shule yake kwa kuiga wengine | Anatunza mazingira ya shule yake kwa ari na kujituma | Anajitolea kutunza mazingira ya shule yake | |
| | | c) Kuiletea sifa shule yake | Vitendo vya kuiletea sifa shule yake vinafanyika ipasavyo | Anafanya vitendo vya kuiletea sifa shule yake kwa shuruti | Anafanya baadhi ya vitendo vya kuiletea sifa shule yake kwa utashi wake | Anafanya vitendo vya kuiletea sifa shule yake ipasavyo | Anawaongoza wenzake kuiletea sifa shule yao | |
| | 1.3 Kuipenda Tanzania kwa kuenzi tunu za nchi na asili yake | a) Kutambua alama za Taifa. | Utambuzi wa alama za Taifa unafanyika kikamilifu | Anatambua alama za Taifa kwa kufanya makosa kidogo | Anatambua alama za Taifa zinazopatikana katika mazingira yake | Anatambua alama za Taifa na kuzielezea vizuri | Anasaidia wenzake kutambua alama za Taifa na kuzielekeza kwa ufasaha | 12 |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | b) Kutambua tunu za Taifa la Tanzania | Utambuzi wa tunu za Taifa la Tanzania unafanyika kikamilifu | Anatambua tunu za Taifa la Tanzania kwa kufanya makosa madogo | Anatambua tunu chache za Taifa la Tanzania | Anatambua tunu za Taifa la Tanzania na kuzielezea vizuri. | Anatambua tunu za Taifa la Tanzania na kuwasaidia wenzake kuzifahamu vizuri. | 12 |
| | | c) Kutambua asili ya nchi ya Tanzania | Utambuzi wa asili ya nchi ya Tanzania unafanyika kikamilifu | Anatambua asili ya nchi ya Tanzania kwa kufanya makosa madogo madogo | Anatambua mambo machache yanayoelezea asili ya nchi ya Tanzania | Anatambua asili ya nchi ya Tanzania kikamilifu. | Anaweza kuelezea asili ya nchi ya Tanzania kwa watu wengine kikamilifu. | |
| 2. Kuthamini jamii | 2.1 Kujijali na kuwajali wengine | a) Kujieleza kwa wenzake na watu wazima anapopatwa na matatizo | Maelezo kwa wenzake na watu wazima anapopatwa na tatizo yanatolewa kwa ufasaha | Anajieleza kwa wenzake na watu wazima anapopatwa na matatizo kwa kuficha baadhi ya mambo | Anajieleza kwa wenzake vizuri lakini anashindwa kujieleza kwa watu wazima anapopatwa na matatizo | Anajieleza kwa ufasaha kwa wenzake na watu wazima anapopatwa na matatizo | Anajieleza kwa wenzake na watu wazima pamoja na kuomba ushauri anapopatwa na matatizo | 12 |
| | | b) Kuepuka vitendo vinavyoweza kuhatarisha usalama wake na jamii. | Vitendo vinavyoweza kuhatarisha usalama wake na jamii vinaepukwa ipasavyo | Anaepuka vitendo vinavyoweza kuhatarisha usalama wake pekee | Anaepuka baadhi ya vitendo vinavyoweza kuhatarisha usalama wake na jamii | Anaepuka vitendo vinavyoweza kuhatarisha usalama wake na jamii ipasavyo | Anaepuka vitendo vinavyoweza kuhatarisha usalama wake na kushauri wenzake kuepuka vitendo hivyo | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kumsaidia mtu mwenye uhitaji | Msaada kwa mtu mwenye uhitaji unatolewa ipasavyo | Anamsaidia mtu mwenye uhitaji kwa kuelekezwa | Anaweza kumsaidia mtu mwenye uhitaji kwa utashi wake | Anaweza kumsaidia mtu mwenye uhitaji ipasavyo bila kuelekezwa | Anamsaidia mtu mwenye uhitaji na kuwashauri wenzake kufanya hivyo | |
| | 2.2 Kutunza mazingira na vilivyomo | a)Kutambua mazingira yanayo mzunguka | Utambuzi wa mazingira yanayo mzunguka unafanyika ipasavyo | Anaweza kubainisha vitu vichache vilivyopo katika mazingira yanayomzunguka | Anaweza kueleza maana ya mazingira yanayomzunguka | Anatambua mazingira yanayomzunguka ipasavyo | Anatambua mazingira yanayomzunguka na kutoa maelezo ya namna ya kuyatunza | 9 |
| | | b) Kuthamini mimea na wanyama | Vitendo vya kuthamini mimea na wanyama vinafanyika ipasavyo | Anatambua matendo machache ya kuthamini mimea na wanyama | Anathamini mimea na wanyama kwa kiwango kidogo | Anathamini mimea na wanyama ipasavyo | Anakemea matendo ya kikatili dhidi ya wanyama na uharibifu wa mazingira | |
| | | c) Kutunza vyanzo vya maji | Utunzaji wa vyanzo vya maji unafanywa kikamilifu | Anatambua matendo ya kutunza vyanzo vya maji lakini hatunzi vyanzo hivyo | Anatunza vyanzo vya maji mara chache | Anatunza vizuri vyanzo vya maji katika maeneo yanayomzunguka | Anatunza vyanzo vya maji na kuwashauri wenzake kutofanya matendo ya kuharibu vyanzo hivyo | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Utendaji wa chini ya wastani** | **Utendaji wastani** | **Utendaji mzuri** | **Utendaji mzuri sana** | |
| | 2.3 Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii | a) Kuwasiliana vyema na wenzake ndani na nje ya darasa | Mawasiliano chanya na wenzake ndani na nje ya darasa yanafanyika kwa ufasaha | Anatumia lugha na matendo yasio faa kuwasiliana na wenzake ndani na nje ya darasa | Anawasiliana vyema na wenzake ndani na nje ya darasa kwa kiwango kidogo | Anawasiliana vyema na wenzake ndani na nje ya darasa kwa ufasaha | Anawashauri wenzake kuwa na mawasiliano mazuri kati yao | 8 |
| | | b) Kushiriki katika kutatua tatizo alilonalo rafiki yake | Ushiriki wake katika kutatua tatizo la rafiki yake unafanyika kikamilifu | Anatambua tatizo linalomkabili rafiki yake lakini hachukui hatua haraka | Anashiriki katika kutatua baadhi ya matatizo aliyonayo rafiki yake kwa haraka | Anashiriki katika kutatua tatizo la rafiki yake kikamilifu | Anashiriki katika kutatua matatizo ya watu mbalimbali | |
| 3. Kuwa mwajibikaji | 3.1 Kulinda rasilimali na maslahi ya nchi | a) Kutambua rasilimali zilizopo katika mazingira yanayo mzunguka | Rasilimali zilizopo katika mazingira yanayomzu nguka zinatambu liwa ipasavyo | Anafahamu maana ya rasilimali | Anataja rasilimali zilizopo katika mazingira yanayomzunguka bila kueleza umuhimu wake | Anatambua rasilimali zilizopo katika mazingira yanayo mzunguka ipasavyo | Anawasaidia wenzake kutambua njia bora za kutunza rasilimali zilizopo katika mazingira yanayowazunguka | 8 |
| | | b) Kulinda na kutunza rasilimali zilizopo katika mazingira | Rasilimali zilizopo katika mazingira yana yomzunguka zinalindwa na kutunzwa ipasavyo | Anafahamu umuhimu wa kulinda na kutunza rasilimali zilizopo katika mazingira yanayomzunguka kwa kiasi kidogo | Analinda na kutunza baadhi ya rasilimali zilizopo katika mazingira yanayo mzunguka vizuri | Analinda na kutunza rasilimali zilizopo katika mazingira yanayomzu nguka ipasavyo | Anawahamasisha wenzake kulinda na kutunza rasilimali zilizopo katika mazingira yao | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 3.2 Kusimamia majukumu yanayomhusu ya nyumbani na shuleni | a) Kutekeleza majukumu yake ya shuleni na nyumbani | Majukumu yake ya shuleni na nyumbani yanatekelezwa kikamilifu | Anatekeleza majukumu machache ya shuleni na nyumbani kwa kushurutishwa | Anatekeleza baadhi ya majukumu yake ya shuleni na nyumbani kwa utashi wake | Anatekeleza majukumu yake ya shuleni na nyumbani kikamilifu | Anawaongoza wengine kutekeleza majukumu yao ya shuleni na nyumbani kikamilifu | 8 |
| | | b) Kusimamia kazi mbalimbali shuleni na nyumbani | Kazi mbalimbali za shuleni na nyumbani zinasimamiwa kikamilifu | Anasimamia baadhi ya kazi za shuleni na nyumbani bila ya ukamilifu | Anasimamia baadhi ya kazi shuleni na nyumbani kwa ukamilifu | Anasimamia kazi mbalimbali shuleni na nyumbani kwa ukamilifu zaidi | Anawaongoza wenzake kusimamia kazi zao za shuleni na nyumbani | |
| | 3.3 Kutii sheria na kanuni katika kutekeleza majukumu yake kila siku | a) Kufahamu sheria na kanuni za shule | Sheria na kanuni za shule zinafahamika ipasavyo | Anataja sheria na kanuni za shule anazozifahamu kwa urahisi | Anafahamu baadhi ya sheria na kanuni za shule | Anafahamu sheria na kanuni zote za shule | Anawa hamasisha wenzake kufahamu sheria na kanuni zote za shule kikamilifu | 8 |
| | | b) Kufuata sheria na kanuni za shule | Sheria na kanuni za shule zinafuatwa kama inavyotakiwa | Anafuata baadhi ya sheria na kanuni za shule kwa kushurutishwa | Anafuata baadhi ya sheria na kanuni za shule bila shuruti | Anafuata sheria na kanuni zote za shule kama inavyotakiwa | Anakuwa mfano mzuri sana na kuwashauri wenzake kufuata sheria na kanuni za shule wakati wote | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Utendaji wa chini ya wastani** | **Utendaji wastani** | **Utendaji mzuri** | **Utendaji mzuri sana** | |
| | 3.4 Kuwa na nidhamu binafsi | a) Kupangilia kazi zake anazofanya | Mpangilio wa kazi zake unafanywa kwa usahihi | Anapangilia kazi zake anazofanya bila mpangilio mzuri | Anapangilia baadhi ya kazi zake anazofanya | Anapangilia kazi zake anazofanya kwa usahihi | Anakuwa mfano wa kuigwa katika kupangilia kazi zake vizuri | 12 |
| | | b) Kujituma katika kazi kwa uwezo wake wote bila ya usimamizi | Kujituma katika kazi kunafanyika kwa kutumia uwezo wake wote bila ya usimamizi | Anafanya kazi kwa usimamizi wa hali ya juu | Anajituma katika baadhi ya kazi kwa kutumia uwezo wake kwa usimamizi mdogo | Anajituma katika kazi zote kwa kutumia uwezo wake wote bila ya usimamizi | Anakua mfano kwa wenzake katika kufanya kazi kwa bidii | |
| | | c) Kupenda kujisomea | Tabia ya kupenda kujisomea inaonyeshwa ipasavyo | Anajisomea bila mpangilio | Anaonesha tabia ya kusoma maandiko machache yanayomvutia | Anapenda kujisomea ipasavyo | Anahamasisha wenzake kupenda kujisomea | |
| | 3.5 Kushiriki-ana katika kutekeleza majukumu ya nyumbani na shuleni | a) Kushirikiana na wenzake katika kufanya shughuli za shuleni na nyumbani | Ushirikiano na wenzake katika kufanya shughuli za shuleni na nyumbani unafanyika wakati wote | Anashirikiana na wenzake katika kufanya baadhi ya shughuli za shuleni na nyumbani kwa kushurutishwa | Anashirikiana na wenzake katika kufanya baadhi ya shughuli za shuleni na nyumbani kwa hiyari bila weledi | Anashirikiana na wenzake katika kufanya shughuli za shuleni na nyumbani wakati wote kwa weledi | Anaongoza wenzake kufanya shughuli za shuleni na nyumbani ipasavyo | 8 |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 4. Kuwa mstahi milivu | 4.1 Kuvumilia katika maisha ya kila siku | a) Kuonesha tabia ya kuwakubali watu wengine jinsi walivyo | Tabia ya kuwakubali watu wengine jinsi walivyo inaoneshwa kikamilifu | Anaonesha tabia ya kuwakubali watu wenye msaada kwake pekee | Anaonesha tabia ya kuwakubali baadhi ya watu | Anaonesha tabia ya kuwakubali watu wengine jinsi walivyo kikamilifu | Anawaongoza wenzake kujenga tabia ya kuwakubali watu wengine jinsi walivyo | 12 |
| | | b) Kufanya vitendo vya kuwavumilia watu wenye haiba tofauti | Vitendo vya kuwavumilia watu wenye haiba tofauti vinafanywa kikamilifu | Anafanya vitendo vichache vya kuwavumilia watu wenye haiba tofauti | Anafanya vitendo vya kuwavumilia watu wenye haiba tofauti | Anafanya vitendo vya kuwavumilia watu wenye haiba tofauti kikamilifu | Anawashauri wengine kufanya vitendo vya kuwavumilia watu wenye haiba tofauti vizuri zaidi | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | c) Kuwasiliana kwa lugha inayofaa pindi anapoudhiwa | Mawasiliano kwa lugha inayofaa pindi anapoudhiwa yanafanyika kikamilifu | Anaanza kutumia lugha inayofaa katika kuwasiliana na watu pindi anapoudhiwa | Anatumia lugha inayofaa katika kuwasiliana na baadhi ya watu pindi anapoudhiwa | Anatumia lugha inayofaa katika kuwasiliana na watu pindi anapoudhiwa kikamilifu | Anawashauri wenzake kutumia lugha inayofaa katika kuwasiliana na watu wanapoudhiwa | |
| | 4.2 Kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya | Kuonesha tabia ya kufanya kazi na kumaliza kwa wakati | Tabia ya kufanya kazi na kuimaliza kwa wakati inaonyeshwa kikamilifu | Anaanza kuonesha tabia ya kupenda kazi | Anaonesha tabia ya kufanya kazi na kumaliza bila ya kuzingatia wakati | Anaonesha tabia ya kufanya kazi na kumaliza kwa wakati | Anawasimamia wengine kufanya kazi na kumaliza kwa wakati | 4 |
| | 4.3 Kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu | Kujifunza maarifa mapya kwa kudadisi mambo mbalimbali | Tabia ya kujifunza maarifa mapya kwa kudadisi mambo mbalimbali inaonyeshwa ipasavyo | Anajifunza maarifa mapya kutokana na mwongozo wa mwalimu pekee | Anajifunza baadhi ya maarifa mapya kwa kudadisi mambo mbalimbali | Anajifunza maarifa mapya kwa kudadisi mambo mbalimbali ipasavyo | Anawashauri wenzake kudadisi mambo mbalimbali ili waweze kujenga umahiri mpya. | 4 |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 5. Kuwa mwadilifu | 5.1 Kuaminika katika jamii | a). Kutenda matendo yanayojenga tabia ya uaminifu | Matendo yanayojenga tabia ya uaminifu yanatendwa kikamilifu | Anabainisha matendo yanayojenga tabia ya uaminifu lakini hatendi matendo hayo | Anatenda baadhi ya matendo ya uaminifu | Anatenda matendo yanayojenga uaminifu kwa watu wote kikamilifu | Anawashauri wenzake watende matendo ya uaminifu kikamilifu | 10 |
| | | b). Kueleza vitendo vinavyovunja uaminifu | Vitendo vinavyovunja uaminifu vinaelezwa kwa usahihi | Anataja baadhi ya vitendo vinavyovunja uaminifu | Anaeleza vitendo vingi vinavyovunja uaminifu | Anaeleza vitendo vinavyovunja uaminifu na kutoa mfano | Anawashauri wenzake kuepuka kutenda vitendo vinavyovunja uaminifu | |
| | | c). Kutambua matendo ya usaliti | Matendo ya usaliti wanayotenda watu yanatambuliwa kwa usahihi | Anabaini baadhi ya matendo ya usaliti | Anaeleza matendo wengi ya usaliti | Anaelezaa matendo ya usaliti na kutoa mifano | Anakemea matendo ya usaliti yanayofanywa na wenzake | |
| | 5.2 Kutimiza majukumu yake kwa uwazi na ukweli | a). Kuonesha tabia ya kuwa mkweli na muwazi | Tabia ya kuwa mkweli na muwazi inaonyeshwa kwa kiwango kikubwa | Anaanza kuonesha matendo ya kuwa mkweli na muwazi | Anatenda baadhi ya matendo machache yenye kuonesha ukweli na uwazi | Anaonesha tabia ya kuwa mkweli na muwazi kwa kiwango kikubwa | Anawashauri wenzake kuwa wakweli na wawazi kila mara | 8 |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | b) Kubaini matendo yanayo dhihirisha tabia ya uongo | Matendo yanayo dhihirisha tabia ya uongo yanabainishwa | Anabaini maana na kutaja baadhi matendo yanayodhihirisha tabia ya uongo | Anabaini matendo mengi yanayodhihirisha tabia ya uongo | Anabaini kikamilifu matendo yanayodhi hirisha tabia ya uongo | Anabaini matendo yanayodhihirisha tabia ya uongo na kuwashauri wenzake kuyaepuka | |
| | 5.3 Kusima-mia haki | a) Kutambua wajibu na haki za mtoto | Wajibu na haki za mtoto zinatambuliwa ipasavyo | Anatambua wajibu na haki za mtoto kwa kukosea | Anatambua baadhi ya wajibu na haki zake | Anatambua wajibu na haki za mtoto ipasavyo | Anasaidia wenzake kutambua wajibu na haki zao | 12 |
| | | b) Kueleza haki za binadamu | Haki za binadamu zinaelezwa kwa ufasaha | Anataja baadhi ya haki za binadamu | Anaeleza baadhi ya haki za binadamu | Anaeleza haki za binadamu kwa kutoa mifano | Anasaidia wengine kuzifahamu haki za binadamu | |
| | | c) Kueleza matendo yasiyo ya haki anayo fanyiwa mtoto | Matendo yasiyo ya haki anayofanyiwa mtoto yanaelezwa ipasavyo | Anataja matendo machache yasiyo ya haki anayofanyiwa mtoto | Anaeleza baadhi ya matendo yasiyo ya haki anayofanyiwa mtoto | Anatambua matendo yasiyo ya haki anayofanyiwa mtoto kwa kutoa mifano mbalimbali | Anashirikiana na wenzake kupinga matendo yasiyo ya haki anayofanyiwa mtoto | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 6. Kudumisha amani | 6.1 Kuchangamana na watu wenye asili tofauti | a) Kutambua asili ya watu waishio Tanzania | Watu wenye asili tofauti waishio Tanzania wanatambuliwa kwa usahihi | Anataja asili ya baadhi ya watu waishio Tanzania | Anaeleza asili ya watu waishio Tanzania | Anatam-bua asili ya watu waishio Tanzania na kutoa mifano | Anashirikiana na wenzake katika kuelewa asili ya watu waishio Tanzania | 12 |
| | | b) Kufanya kazi pamoja bila kujali tofauti za asili ya mtu | Kazi inafanyika kwa pamoja bila kujali tofauti za asili ya watu kikamilifu | Anafanya kazi kwa pamoja na watu wa asili yake | Anafanya kazi pamoja na baadhi ya watu kujali tofauti za asili yao | Anafanya kazi kwa pamoja bila kujali tofauti za asili ya mtu kikamilifu | Anashauri wenzake kufanya kazi na watu wote bila kujali tofauti za asili ya mtu | |
| | | c) Kutenda matendo yenye kudumisha upendo na amani miongoni mwa watu wa asili tofauti | Matendo yenye kudumisha upendo na amani miongoni mwa watu wa asili tofauti yanatendwa ipasavyo | Anatenda matendo yenye kudumisha upendo na amani kwa watu wa asili yake pekee | Anatenda matendo machache yenye kudumisha upendo na amani miongoni mwa watu wa asili tofauti | Anatenda matendo yenye kudumisha upendo na amani miongoni mwa watu wa asili tofauti | Anashauri wenzake kutgenda matgendo yenye kudumisha upendo na amani miongoni mwa watu wa asili tofauti | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | 6.2 Kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitaza-mo mion-goni mwa watu wa jamii tofauti | a) Kueleza dhana ya utamaduni | Dhana ya utamaduni inaelezwa kwa usahihi | Anataja vitu vichache vinavyounda utamaduni | Anaeleza maana ya utamaduni | Anaeleza dhana ya utamaduni kwa kutoa mifano | Anaelezea wenzake dhana ya utamaduni kwa kutoa mifano ya vitu vinavyounda utamaduni | 12 |
| | | b) Kuonesha tabia ya kujifunza tamaduni za makabila tofauti | Tabia ya kujifunza tamaduni za makabila tofauti inaoneshwa kikamilifu | Anaonesha tabia ya kujifunza mambo machache kuhusu kabila lake | Anaonesha tabia ya kujifunza tamaduni za kabila lake na makabila mengine machache | Anaonesha tabia ya kujifunza tamaduni za mak-abila tofauti kikamilifu na kuthamini | Anawahamasisha wenzake kujifunza tamaduni za makabila tofauti | |
| | | c) Kukemea mila na desturi potofu | Mila na desturi potofu zinakemewa ipasavyo | Anabaini baadhi ya mila na desturi potofu | Anakemea baadhi ya mila na desturi potofu | Anakemea mila na desturi potofu ipasavyo | Anawaongoza wenzake kukemea mila na desturi potofu kikamilifu | |
| | 6.3 Kujenga urafiki mwema na mataifa mengine | a) Kutofautisha rafiki anayefaa na asiyefaa | Tofauti kati ya rafiki anayefaa na asiyefaa zinabainishwa kwa usahihi | Anaanza kutofautisha rafiki anayefaa na asiyefaa | Anabainisha sifa za rafiki anayefaa na asiyefaa | Anatofautisha rafiki anayefaa na asiyefaa kwa usahihi na kutoa mifano | Anashauri wenzake kuchagua rafiki anayefaa | 7 |
| | | b) Kutambua nchi rafiki na Tanzania | Nchi rafiki na Tanzania zinatambuliwa kwa usahihi | Anataja nchi chache rafiki na Tanzania | Anataja nchi rafiki na Tanzania na kueleza kwa makosa maeneo ya ushirikiano | Anatambua nchi rafiki na Tanzania na kueleza kwa ufasaha aina ya ushirikiano | Anaeleza umuhimu wa Tanzania kuwa na nchi rafiki | |

## 3.8 Darasa la IV

**Jedwali Na. 4:** Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi Darasa la IV

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 1. Kuheshimu jamii | 1.1 Kujipenda na kuwapenda watu wengine<br>1.2 Kuipenda na kujivunia shule yake<br>1.3 Kuipenda Tanzania kwa kuenzi tunu za nchi na asili yake |
| 2. Kuithamini jamii | 2.1 Kujijali na kuwajali wengine<br>2.2 Kutunza mazingira na vilivyomo<br>2.3 Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii |
| 3. Kuwa mwajibikaji | 3.1 Kulinda rasilimali na maslahi ya nchi<br>3.2 Kusimamia majukumu yanayomhusu nyumbani na shuleni<br>3.3 Kutii sheria na kanuni mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku<br>3.4 Kuwa na nidhamu binafsi<br>3.5 Kushirikiana katika kutekeleza majukumu ya nyumbani na shuleni |
| 4. Kuwa mstahimilivu | 4.1 Kuvumilia katika maisha ya kila siku<br>4.2 Kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya<br>4.3 Kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu |
| 5. Kuwa mwadilifu | 5.1 Kuaminika katika jamii<br>5.2 Kutimiza majukumu yake kwa uwazi na ukweli<br>5.3 Kusimamia haki |
| 6. Kudumisha amani | 6.1 Kuchangamana na watu wenye asili tofauti<br>6.2 Kubaini tofauti za kiutamaduni na mtazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti<br>6.3 Kujenga urafiki mwema na mataifa mengine |

**Jedwali Na. 5: Maudhui ya darasa la IV**

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| 1. Kuheshimu jamii | 1.1 Kujipenda na kuwapenda watu wengine | a) Kubainisha vitendo visivyofaa kumtendea mtu yeyote | Vitendo visivyofaa kumtendea mtu yeyote vinabainishwa ipasavyo | Anabainisha vitendo anavyopenda kutendewa | Anabainisha vitendo vichache visivyofaa kumtendea mtu yeyote | Anabainisha vitendo visivyofaa kumtendea mtu yeyote ipasavyo | Anashirikisha wenzake katika kubaini vitendo visivyofaa kuwatendea watu | 13 |
| | | b) Kutenda shughuli mbalimbali kwa kuzingatia mwongozo anaopewa na walimu, wazazi/walezi | Mwongozo anaopewa na walimu, wazazi/walezi unazingatiwa ipasavyo katika kutenda shughuli mbalimbali | Anatenda shughuli mbalimbali bila kuzingatia mwongozo anaopewa na walimu, wazazi/walezi | Anatenda shughuli mbalimbali kwa kuzingatia mwongozo anaopewa na walimu, wazazi na walezi lakini anashindwa kuzingatia baadhi ya maeneo | Anatenda shughuli mbalimbali ipasavyo kwa kuzingatia mwongozo anaopewa na walimu, wazazi/walezi | Anashauri wenzake juu ya umuhimu wa kutenda shughuli mbalimbali kwa kuzingatia mwongozo anaopewa na walimu, wazazi/walezi. | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | d) Kubaini matendo yanayo jitokeza katika jamii ambayo yanaha tarisha usalama wake | Matendo yanayojitokeza katika jamii ambayo yanahatarisha usalama wake yanabainishwa kwa usahihi | Anabainisha baadhi ya matendo yana yohatarisha usalama wake | Anabaini matendo yanayojitokeza katika jamii ambayo yanahatarisha usalama wake | Anabaini matendo yanayojitokeza katika jamii ambayo yanahatarisha usalama wake na kuyaelezea | Anawasaidia wengine kubaini matendo yanayojitokeza katika jamii ambayo yanahatarisha usalama wao | |
| | 1.2 Kuipenda na kujivunia shule yake | a) Kutambua muundo wa uongozi katika shule yake | Muundo wa uongozi wa shule unatambuliwa kwa usahihi | Anataja viongozi wa shule lakini hatambui muundo wa uongozi wa shule yake | Anatambua sehemu ya muundo wa uongozi wa shule yake | Anatambua muundo wa uongozi katika shule yake na kutaja viongozi husika | Anawasaidia wenzake kutambua muundo wa uongozi wa shule na kuwatambua viongozi husika | 9 |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Utendaji wa chini ya wastani** | **Utendaji wastani** | **Utendaji mzuri** | **Utendaji mzuri sana** | |
| | | b) Kuzingatia sheria na kanuni za shule yake | Sheria na kanuni za shule zinazingatiwa ipasavyo | Anazingatia baadhi ya sheria na kanuni za shule kwa kushurutishwa | Anazingatia baadhi ya sheria na kanuni za shule kwa hiyari bila shuruti | Anazingatia sheria na kanuni za shule yake | Anahamasisha wenzake kuzingatia sheria na kanuni za shule mara zote | |
| | | c) Kushiriki katika shughuli zenye kuiletea sifa shule yake | Ushiriki wake katika shughuli zenye kuiletea sifa shule yake unafanyika kikamilifu | Anabainisha shughuli zenye kuiletea sifa shule yake | Anashiriki katika shughuli chache zenye kuiletea sifa shule yake | Anashiriki kikamilifu katika shughuli zenye kuiletea sifa shule yake | Anawahimiza wenzake kushiriki katika shughuli zenye kuiletea sifa shule yake | |
| | 1.3 Kuipenda Tanzania kwa kuenzi tunu za nchi na asili yake | a) Kuchora alama za Taifa | Alama za Taifa zinachorwa kwa usahihi kwa kuzingatia mpangilio wake | Anachora alama za Taifa kwa kukosea sana | Anachora alama za Taifa kwa usahihi bila kuzingatia mpangilio wa rangi | Anachora alama za Taifa kwa usahihi kwa kuzingatia mpangilio wa rangi | Anawaelekeza wenzake kuchora alama za Taifa na kueleza umuhimu wake | 13 |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa chini ya wastani | Utendaji wastani | Utendaji mzuri | Utendaji mzuri sana | |
| | | b) Kuthamini alama za Taifa | Alama za Taifa zinathaminiwa ipasavyo | Anatambua alama za Taifa lakini anashindwa kuzithamini | Anathamini alama chache tu za Taifa | Anathamini alama za Taifa na kutoa maelezo | Anawaeleza wenzake umuhimu wa kuthamini alama za Taifa | |
| | | c) Kubainisha dhana ya demokrasia | Dhana ya demokrasia inabainishwa kwa usahihi | Anabaini baadhi ya vitu vinavyojenga demokrasia | Anabainisha dhana ya demokrasia | Anabainisha dhana ya demokrasia na kutoa maelezo ya mambo yanayojenga demokrasia | Anawaelimisha wenzake juu ya umuhimu wa demokrasia | |
| | | d) Kutambua muundo wa serikali ya kijiji / mtaa | Muundo wa serikali ya kijiji/mtaa unatambuliwa kwa usahihi | Anatambua viongozi wa serikali ya kijiji/ mtaa | Anatambua ngazi chache za muundo wa serikali ya kijiji/ mtaa | Anatambua muundo wa serikali ya kijiji/ mtaa na kutoa maelezo | Anawasaidia wengine kutambua muundo wa serikali ya kijiji/ mtaa | |
